

# TANGAZO

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Babati anawatangazia Watumishi kuwa Ofisi yake imepanga kutoa Mikopo Kwa Watumishi Wa Umma Kupitia Wizara ya Fedha na Mipango.

Serikali kupitia Mikopo hiyo inawawezesha Watumishi wake kwa kuwakopesha Fedha taslimu kwa ajili ya kununua magari/pikipiki kwa ajili ya usafiri

Watumishi wenyewe sifa na uhitaji wa mkopo huo wawasllishe maombi yao kwa Mkurugenzi Mtendaji yakiambatana na fomu za maombi.

## SIFA ZA MUOMBAJI

- I. Awe ni Mtumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati
- II. Mshahara wake halisi uwe unazidi 1/3;
- III. Awe na mwenendo mwema katika utumishi wa umma ;
- IV. Awe amethibitishwa kazini;
- V. Awe hajawahi kukopeshwa mkopo huu na
- VI. Awe analipwa Mshahara kupitia fungu Vote 70A4 kutoka Serikali kuu

## MASHARTI YA MKOPO

- I. Mwombaji aambatishe katika barua yake maombi, Mtu wake wa karibu (Next of kin) kwa kuambatisha/ kuonesha taarifa zifuatazo:-
  - a) Majina matatu halisi na majina maarufu;
  - b) Uhusiano wake;
  - c) Kitambulisho cha Taifa (NIDA);
  - d) Anwani ya kudumu;
  - e) Mkoa anakoishi, Wilaya, Kata, Kijiji/ Mtaa;
  - f) Namba za simu iliyosajiliwa kwa majina halisi
  - g) Anwani ya Barua pepe (Email Address);

**NB:** Next of kin ina maana ya mtu wako wa karibu mwenye umri kuanzia miaka 18 ambaye anaweza kutoa taarifa zako kwa usahihi.

- II. Mkopo utatolewa kwa kuzingatia kiwango kulingana na ngazi ya mshahara na salio la 1/3 ya mshahara;
- III. Mwombaji ajaze fomu tatu halisi za maombi akiambatisha hati tatu (3) (salary slip) za mshahara wa mwezi Desemba 2022 ;Januari 2023 na Februari 2023

- Mwombaji atalipa service charge asilimia tatu na protection fund asilimia moja ya Mkopo atakaopewa;
- Marejesho ya Mkopo yatalipwa kuitia makato ya mshahara wa mkopajī isipokuwa kama itaelekezwa vinginevyo;
- VI. Mkopajī atatakiwa kulipa mkopo huo wote kwa muda ambao umekubaliwa na pande zote, muda hautazidi miezi 72;
- VII. Mkopo wa Mtumishi utafutwa ikiwa
- a) Atakoma Utumishi wake kwa sababu za ugonjwa
  - b) Atafariki
  - c) Atastaafishwa kwa manufaa ya Umma;
- VIII. Mkopajī ana wajibu wa kuuliza taarifa zote zinazohusu mkopo
- IX. Mkopajī anawajibika kutoa taarifa kwa Mkurugenzi Mtendaji endapo makato ya Mshahara wake hayajaanza au yamesimama kinyume cha Mkataba.
- X. Mkopajī anawajibika kuhakikisha amelipa service charge 3% na Bima ya Mkopo (protection Fund) 1%

### **MUDA WA MAOMBI**


Maombi yataanza kupokelewa kuanzia tarehe 27, Februari 2023 hadi 12, Mwezi Machi, 2023 saa 9:30 Alasiri

Maombi yatakayokiuka sifa na masharti ya Mkopo hayataidhinishwa.

Kwa ufanuzi wasiliana na Afisa Utumishi Cosmas S. Quintine

Na za Simu: 0782 515 076/0657515076

Wote Mnakaribishwa



*Benedict Sylvester Ntabagi*

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
BABATI**